



**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU
NYERERE**



**KONGAMANO LA KUMBUKIZI YA KUZALIWA MWALIMU JULIUS K. NYERERE
LITAKALOFANYIKA TAREHE 11 APRILI 2025 KATIKA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA
MWALIMU NYERERE**

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere anapenda kuwaalika Viongozi na Wananchi mbalimbali kushiriki katika Kongamano Maalumu la kumkumbuka Muasisi wa Chuo na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kongamano hilo litafanyika siku ya **Ijumaa Tarehe 11, Mwezi wa Nne mwaka wa 2025** lenye **MADA KUU** isemayo: **"MAONO YA BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS NYERERE KATIKA ELIMU, UWEKEZAJI NA UJENZI WA TAIFA LENYE AMANI KWA MAENDELEO YA WATU.**

Lengo la Kongamano hilo ni kumuenzi Baba wa Taifa katika mambo aliyopigania na kuyasimamia. Mada **TATU** ndogo zitawasilishwa na watoa mada kama ifuatavyo:

Mada ya **KWANZA**; Uwekezaji wenye tija katika kuleta Maendeleo ya Watu. **Mada ya PILI** itahusu Amani, Maridhiano, na Ustahmilivu katika Ujenzi wa Taifa imara kwa Maendeleo ya Watu na Mada ya **TATU** itahusu Mchango wa Elimu ya Kujitegemea katika Ajira na Maendeleo ya Uchumi.

Mwenyekiti wa mjadala wa Kongamano atakuwa, Spika Mstaafu mhe. Anne Makinda **na Mgeni rasmi** wa Kongamano hilo ni **Mhe. Dkt. Dotto Biteko Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Kongamano hilo litafanyika katika ukumbi wa Jengo la Utamaduni, kuanzia saa tatu Asubuhi.